

HALMASHAURI YA WILAYA YA MANYONI

Tarehe 07/09/2019

TANGAZO

Msimamizi wa Uchaguzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni anawatangazia Watumishi wa Umma wote nafasi za kazi kwa ajili ya shughuli za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika tarehe **24 Novemba,2019.**

1. **Nafasi zinazotangazwa:-**

- | | | |
|-----|--|---------------------|
| (a) | Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kata | - Nafasi 19 |
| (b) | Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kijiji | - Nafasi 58 |
| (c) | Msimamizi Msaidizi wa Uchaguzi ngazi ya Kituo | - Nafasi 558 |
| (d) | Waandikishaji wa Wapiga kura | - Nafasi 279 |

2. **Sifa zinazotakiwa** kwa mujibu wa Kipengele Na.6.0 (6.2 a-c) cha Mwongozo wa Uchaguzi wa Viongozi wa ngazi za Vijiji,Vitongoji na Mitaa utakaofanyika tarehe 24 Novemba,2019 ni kama ifuatavyo:-

- (a) Wasiwe na dhamana au uongozi katika chama chochote cha siasa
(b) Wawe ni Watumishi katika Utumishi wa Umma (Public Service).
(c) Wawe Waadilifu.

3. **Malipo kwa ajili ya kazi**

Malipo yatatolewa kulingana na siku za kufanya kazi tu kwa kiwango cha **Tsh.20,000/= kwa siku.**

4. **Namna ya kuandika barua**

- Barua zote ziandikwe kwa mkono
- Barua iandikwe majina kamili yanayotumika katika Utumishi
- Barua itaje nafasi ya kazi unayoomba.
- Barua itaje cheo katika Utumishi wa Umma
- Barua itaje kituo cha kazi
- Barua iwe na anuani kamili ikiwa na namba ya simu
- Barua iambatishwe na CV
- Barua ziwasilishwe kwa mkono masijala ya wazi ya Mkurugenzi Mtendaji Manyoni
- Barua iandikwe kwa:

Msimamizi wa Uchaguzi, Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni,
S.L.P 60, **MANYONI.**

5. **Mwisho**

Mwisho wa kupokea barua hizo ni tarehe 13 Septemba,2019 siku ya Ijumaa saa 9.30 Alasiri.

Imetolewa na:



Charles Edward Fussi
Msimamizi wa Uchaguzi
MANYONI

**MSIMAMIZI WA
UCHAGUZI MANYONI**